

Muhtasari wa Usaidizi wa Kifedha kwa Huduma za Dharura za Hospitali au Huduma za Matibabu Zinazohitajika za Kiafya

Kwa zaidi ya karne moja, urithi wa imani wa Norton Healthcare umeelekeza lengo lake la kuwajali wagonjwa na waliojeruhiwa katika jamii yetu. Urithi huo wa imani unaathiri kila sehemu ya huduma tunazotoa. Hospitali za Norton Healthcare zinatoa huduma za bure au kwa punguzo kwa wagonjwa ambao hawawezi kumudu kulipia na kustahiki kulingana na kipato, rasilimali na hali ya familia. Muhtasari huu unatoa maelezo mafupi ya Sera yetu ya Usaidizi wa Kifedha kwa huduma za dharura za hospitali na matibabu yanayohitajika ya kiafya.

Je, ni nani anastahiki kupata usaidizi wa kifedha?

Iwapo una kipato na/au rasilimali ndogo, huna bima ya afya au una deni lililosalia baada ya bima ya afya, unaweza kustahiki kupata huduma za dharura au huduma za afya bila malipo au kwa punguzo kulingana na vigezo vifuatavyo:

1. Huna bima ya afya au una deni lililosalia baada ya bima ya afya kulipa au kukataa madai; na
2. Hustahiki kwa bima iliyo na ruzuku au msaada wa serikali kama Malipo ya Huduma ya Matibabu kwa Watu Wasiojiweza (DSH), Mpango wa Bima za Afya kwa Watoto (CHIP), Medicaid, Shirika la Huduma za Utunzaji za Medicaid (MCO) au Hoosier Healthwise; na
3. Mapato ya kitengo cha familia yako ni sawa na au chini ya asilimia 350 ya Miongozo ya Shirikisho Kuhusu Umaskini ("FPG"); na
4. Rasilimali (mali) ya kitengo cha familia ya mgonjwa ni sawa au chini ya asilimia 200 ya miongozo ya DSH; na
5. Ili kustahiki usaidizi kwa Hitaji Muhimu la Kimatibabu usio wa dharura, ni lazima pia uwe mkaazi wa Kentucky, Indiana, Tennessee, Ohio au Illinois. Sharti hili la makazi halitumiki kwa Huduma ya Dharura.

Sera ya Usaidizi wa Kifedha pia inaelezea vigezo vingine vinavyostahiki huduma fulani.

Je, nitatozwa kiasi gani kwa huduma?

Norton Healthcare inatoa huduma za dharura na huduma nyinginezo za kiafya zinazohitajika katika hospitali bila malipo kwa wagonjwa wote wanaokidhi vigezo vya usaidizi chini ya sera hii. Wagonjwa wanaofaa kupata msaada wa kifedha hawatowzi zaidi ya kiasi kilichofungamanishwa kwa jumla na wagonjwa walio na bima. Hii inajumuisha huduma kwa hospitali nane za Norton Healthcare, Kituo cha matibabu cha watoto cha Norton — Brownsboro, Taasisi ya Saratani ya Norton, Vituo vya Uchunguzi vya Norton na Vituo vya uchunguzi vya Moyo vya Norton.

Je, ni vipi nitaweza kuomba msaada?

Ili kutuma ombi la usaidizi wa kifedha, lazima ujaze maombi yaliyoandikwa na utoe taarifa za benki za miezi 3 iliyopita kwa kila akaunti ya hundi na akiba. Huenda ukalazimika kutoa nakala ya kulipa kodi ya mwaka uliopoita na hati nyinginezo, kama inavyohitajika katika Sera ya Usaidizi wa Kifedha.

Je, nitawezaje kupata nakala za sera ya usaidizi wa kifedha na fomu ya kutuma ombi?

Hati za Sera ya usaidizi wa kifedha na fomu za kutuma maombi za Hospitali ya Northcare zinapatikana bure kwa www.NortonHealthcare.com/FAP na katika ofisi zote za Norton zinazotoa huduma za ushauri na idara za huduma za dharura. Au unaweza kupiga simu kwa huduma kwa mteja kwa (502) 479-6300 ili uombe utumiwe taarifa hizi kupitia baruapepe bila malipo.

Je, ninawezaje kujifunza zaidi kuhusu Sera ya Usaidizi wa Kifedha na kupata usaidizi wa mchakato wa kutuma ombi?

Kujifunza mengi kuhusu Sera ya Usaidizi wa Kifedha na mchakato wa kutuma ombi, wasiliana na mshauri wa kifedha anayepatikana kwenye hospitali zetu, au mpigie mtoaji huduma kwa wateja kwa 502-479-6300.

Je, itakuwaje ikiwa sitimizi mahitaji ya kupata usaidizi chini ya sera hii?

Iwapo hutimizi mahitaji ya sera zetu za Usaidizi wa Kifedha kwa huduma za dharura au huduma za matibabu ya kiafya zinazohitajika, au kutafuta msaada wa huduma zisizo za dharura au ambazo zinahitajika kiafya, bado

unaweza kupata punguzo kupitia kwa mpango tofauti iwapo huna bima ya afya. Piga simu kwa huduma kwa wateja kupitia (502) 479-6300 ili kujifunza mengi zaidi.

Sera za Usaidizi wa Kifedha na kutuma maombi, huu ni muhtasari wa sera hiyo, na hati nyingine zinazohusiana zinapatikana katika lugha za Kihispania, Serbo-Kikroatia, Kivietinamu na Kiarabu.